

Simu: +255677003373  
E mail :td@nzegatc.go.tz  
Tovuti:www.nzegatc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji,  
S.L.P. 256,  
NZEGA –TABORA.

19/01/2018

### **TAARIFA KWA UMMA**

Katibu Tawala Mkoa wa Tabora ametoa pongezi kubwa kwa uongozi wa Halmashauri ya Mji Nzega kufuatia ushiriki wa wanafunzi, Walimu na Maafisa michezo katika mashindano ya **Olimpiki Maalum kwa Wanafunzi wenye ulemavu wa akili yaliyofanyika Mjini Magharibi Mwezi Disemba 2017 katika uwanja wa Amaan Mjini Zanzibar**

Katika barua yake hiyo Katibu Tawala alieleza kuwa pongezi hizi zinatokana na jitihada zilizowawezesha washiriki kutoka Mkoa wa Tabora kuweza kuleta tuzo za medali ya **dhahabu 6** na medali ya **fedha 7** na kufanya jumla ya **medali 13**.

Aidha Katibu tawala ametoa pia rai kuendelea kujiandaa vyema na michezo mingine kama UMISETA na UMITASHUMTA ili Mkoa wetu upate tuzo nyingi zaidi kuzidi hizi.

Wakati huo huo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Nzega amepokea tuzo hizo kutoka kwa Afisa Michezo wa Halmashauri ya Mji Nzega aliyeshiriki katika mashindano hayo. Akipokea tuzo hizo, Mkurugenzi amempongeza Afisa michezo kwa kazi kubwa aliyofanya na kufanya Halmashauri ya Mji Nzega kung'ara. Amewapongeza pia wanafunzi wa Shule ya Msingi Kitongo pamoja na Walimu wao kwa maandalizi mazuri kwa wanafunzi hao yaliyowawezesha kushiriki vizuri kwenye mashindano na hatimaye kurudi na tuzo. Amewataka kuendelea na juhudi hizo hizo na kuhakikisha kuwa tunaendelea kushiriki katika mashindano hayo na kupata tuzo nyingi zaidi.

Michezo ni afya, urafiki na ajira. Hongereni sana kwa hatua hiyo na ongezeni jitihada zaidi.

Imetolewa na kitengo cha TEHAMA.

**HALMASHAURI YA MJI NZEGA**